



**Lengo>> Kuongeza tija ya nyama zinazozalishwa**

# Serikali kutumia sh. milioni 600 kukarabati mabwawa ya mifugo

**Na WARIOBA YGOMBE, Morogoro**

SERIKALI imesema itatumia zaidi ya sh. milioni 900, kufanya ukarabati mkubwa wa mabawa mawili ya kunyweshea mifugo yaliyoko katika mikoa ya Manyara na Arusha ili kuongeza tija ya mifugo nchini.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel na kuongeza kuwa, serikali imeamua kutumia fedha hizo kukarabati Bwawa la Narakau lililoko Manyara na Kimokuwa la Arusha.

"Tumeamua kufanya ukarabati wa mabwawa mawili yaliyoko ili kuongeza thamani ya mifugo ya wafugaji wetu na kuleta tija ya nyama zinazozalishwa

Narakau, limetengewa sh. milioni 413 wakati la Kimokuwa likitengewa sh. milioni 511.9 kwa lengo la kuongeza tija.

Mbali na ukarabati wa mabwawa hayo, alisema miradi kama hiyo ya ukarabati wa mabwawa ya kunyweshea mifugo, inaendelea pia katika kata ya Chamakweza, Chalinze mkoani Pwani na Kata ya Mbangala, mkoani Songwe.

Profesa Ole Gabriel, alisema mradi wa ukarabati wa mabwawa hayo upo katika hatua za kukamikia, ambapo wizara yake itaendelea kuboresha upatikanaji wa maji ili wafugaji waondokane na changamoto ya kutembea umbali mrefu.

Profesa Ole Gabriel, alitaka Kampuni ya Ujenzi ya Zoco iliyopewa

mawili na kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Kwa upande wao, wafugaji walisema uamuzi wa serikali wa kujenga mabwawa maeneo hayo, umeonesha jinsi inavyothamini wafugaji nchini na kwamba, kukamilika kwake kutaongeza thamani ya mifugo.

Kasaine Lamaiba, alisema ujenzi wa mabwawa utasaidia pia visima vya asili kutumika kwa muda mrefu bila kukauka kwa sababu kutakuwa na vyanzo mbalimbali vya maji na ya uhakika.

Petro Narotoka, aliziomba halmashauri husika kutoa ushirikiano ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati huku akiwasihi wafugaji wenzake kutunza miundombinu hivo ili iweze